

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

**TUME YA UCHUNGUZI WA KIJINAI WA MATUKIO YA GHASIA YA  
WAKATI NA BAADA YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025**

---

Katika kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Rais ya Kuchunguza Matukio ya Uvunjifu wa Amani Yaliyotokea Wakati na Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025 na kwa kuzingatia mamlaka aliyonayo chini ya Sheria ya Tume za Uchunguzi, Sura ya 32, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameunda Tume ya Uchunguzi wa Kijinai wa Matukio ya Ghasia ya Wakati na Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Aidha, Mhe. Shabani Ally Lila, Jaji wa Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameteuliwa kuwa Kamishna na Mwenyekiti wa Tume na wafuatao wameteuliwa kuwa Makamishna wa Tume hiyo:-

- (i) Mhe. Gad John Mjemmas - Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania;
- (ii) Mhe. Awadh Mohamed Bawazir - Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania; na
- (iii) Mhe. Aishieli Nelson Sumari - Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

Imetolewa na Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi,

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Moses M. Kusiluka'.

**Balozzi Dkt. Moses M. Kusiluka**  
**KATIBU MKUU KIONGOZI**

18 Mei, 2026